

Kutumia mwakilishi wa masuala ya uhamiaji—Fanya inavyofaa

Nchi ya Canada inawakaribisha maelfu ya wageni kila mwaka. Wengi wanachagua kutumia mwakilishi wa kulipwa awasaidie katika maombi yao ya uhamiaji na uraia.

Watu wanaotoa ushauri au uwakilishi wa masuala ya uhamiaji au uraia kwa malipo **lazima** waidhinishwe. Hii inamaanisha kwamba kutoa uwakilishi au ushauri wa masuala ya uhamiaji kwa malipo inaweza kufanywa tu na wanachama wenyewe kibali kutoka moja ya vyombo vifuatavyo:

- chama cha sheria cha eneo au mkoa wa Kanada
- Chambre des notaires du Québec
- College of Immigration and Citizenship Consultants

Ukiamua kuajiri **mshauri** wa masuala ya uhamiaji au uraia, **lazima awe na kibali**. Kuanzia Novemba 23, 2021, College of Immigration and Citizenship Consultants ndiye msimamizi rasmi wa washauri wa masuala ya uhamiaji na uraia. Immigration, Refugees and Citizenship Canada (IRCC) **haitapokea maombi yanayowasilishwa na washauri wasio na kibali**.

Chagua mwakilishi kwa umakini

- Waombe watu unaowaamini wampendekeze mtu. Pata ushauri kutoka kwa watu kadhaa kabla ya kuchagua.
- Tafuta mwakilishi mwenye kibali kuitia tovuti ifuatayo Canada.ca/immigration-representative.
- Ulizia kuhusu mafunzo na uzoefu wa mwakilishi. Kwa mfano, omba marejelezo na chunguza amekuwa akifanya biashara hii kwa muda gani. Kuwa makini na mtu ambaye hatajibu maswali yako.
- Thibitisha kwamba [mwakilishi ameidhinishwa](#).

Baada ya kuchagua mwakilishi chukua hatua zifuatazo:

- Omba **mkataba wa maadhishi (au makubaliano ya huduma)** na usome kwa umakini kabla ya kusaini. Hakikisha mkataba huo umeorodhesha huduma ambazo mwakilishi atakupatia (kama vile kutoa ushauri wa masuala ya uhamiaji au kushughulika na IRCC kwa niaba yako). Mkataba huo unapaswa kuainisha wazi wazi ada yake.
- Kuwa makini na mwakilishi anayependekeza utoe taarifa za uongo au ufiche taarifa fulani kwenye maombi yako. Hii ni kinyume na sheria. Inaweza kusababisha maombi yako kukataliwa, kuzuiwa kuingia nchi ya Canada, au kuhamishwa nchini baada ya kuwasili.
- Usisaini fomu za maombi ambazo hazijajazwa, au fomu au nyaraka zozote ambazo huwezi kuzisoma. Ikiwa huzielewi, omba mtu akusaidie.
- Ombo nakala za nyaraka zozote anazokuandalia mwakilishi wako.
- Ombo risiti iliyosainiwa unapomlipa mwakilishi wako.
- Linda pesa zako na kumbuka kwamba IRCC:
 - haitakuomba **kamwe** uweke fedha kwenye akaunti binafsi ya benki au uhamishe fedha kuitia kampuni binafsi ya kuhamisha fedha
 - [inapokea ada](#) katika dola ya Canada, na hazitofautiani ulimwenguni kote. Ada katika sarafu mahalia zinashughulikiwa kulingana na viwango rasmi ya kubadilisha fedha.

Ikiwa una tatizo na mwakilishi wako, unaweza kufungua lalamiko.

- **Kwa mshauri wa masuala ya uhamiaji au uraia**, wasiliana na [College of Immigration and Citizenship Consultants](#).
- **Kwa mwanasheria au mthibitishaji wa hati za kisheria**, wasiliana na [Canadian provincial or territorial law society](#) au [Chambre des notaires du Québec](#) (kwa Kifaransa tu).
- **Kwa msaidizi wa kisheria (Ontario tu)**, wasiliana na [Law Society of Ontario](#).

Kwa dondoa nyingine muhimu, orodha ya wawakilishi walioidhinishwa, na taarifa za jumla ili kukusaidia kuchagua mwakilishi, tembelea tovuti ifuatayo [Canada.ca/immigration-representative](https://www.canada.ca/en/immigration-refugees-citizenship/corporations-businesses-immigration/immigration-representatives.html).